**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KISHAPU**

Simu: 0282770020,
Nukushi: 0282770019,
Barua pepe: info@kishapudc.go.tz
Tovuti: www.kishapudc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
S.L.P. 1288,
22Barabara ya DED-DC
**37582 KISHAPU.**

*Unapojibu Tafadhali Taja:-*

Kumb.Na.HA.54/101/01/47 **13/02/2026**

---

## TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA ZA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Wilaya ya Kishapu anawatangazia Watanzania wenye sifa ya kuomba kazi za mkataba (Contracts terms) nafasi Mbili (2) katika Hospitali ya Jakaya Mrisho Kikwete na Hospitali ya Wiliamson Diamond.

### 1.1 MTEKNOLOJIA DARAJA LA II (RADIOLOJIA NA MIONZI) - NAFASI 2

#### 1.1.1 MAJUKUMU / KAZI

i. Kuwapima wagonjwa wanaoelekezwa kwenye eneo lake la kazi.
ii. Kutunza mitambo na vifaa vya Radiolojia katika eneo la kazi.
iii. Kukagua picha za X-Ray zilizopimwa kwa ubora na kutosheleza (Radiolojistc Quality).
iv. Kutunza picha za wagonjwa hadi majibu yanapowafikia madaktari waliowatunza wagonjwa.
v. Kusimamia watumishi walio chini yake.
vi. Kutoa ushauri kuhusu masuala ya kazi za Radiolojia na Mionzi katika eneo lake la kazi.
vii. Kuandaa vifaa vya Tiba/Uchunguzi na kusimamia utakasaji vifaa katika eneo la kazi (Sterilization).
viii. Kutoa mafunzo ya awali kwa watumishi wanaopangiwa kazi katika eneo lake la kazi.
ix. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

#### 1.1.2 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye Stashahada (Diploma) katika fani ya Uteknolojia (Radiolojia na Mionzi) katika moja ya fani zilizotajwa hapo juu, kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza pale inapohusika.

#### 1.1.3 NGAZI YA MSHAHARA

**TGHS B**

**MASHARTI YA JUMLA**

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri wa kuanzia miaka18 na usiozidi miaka 45

ii. Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detail Curriculum Vitae) yenye anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana na Anuani ya Barua Pepe (E-mail address) pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.

iii. Maombi yote yaambatane na nakala ya vyeti vya Elimu na Taaluma Pamoja na cheti cha kuzaliwa vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne/Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika. **Diploma/Certificates, - Cheti cha mtihani wa Kidato cha IV na VI, - Vyeti vya Kitaaluma.**

iv. "Testmonial ", "Provisional Results ", "Statement of results ", hati ya matokeo ya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita (**FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**

viii. Waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na vimethibitishwa na Mamlaka husika **(TCU, NECTA na NACTE**).

ix. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

x. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

xi. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **01 Machi, 2026.**

xii. **MUHIMU:** Kumbuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa na ielekezwe kwa anuani ya; -

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu,
22 Barabara ya DED-DC
S.L.P 1288,
**37582 KISHAPU.**

i. Maombi yote yatumwe kwa njia ya POSTA au Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya katika Masijala ya Wazi.

ii. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioanishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKILIWA.**

Tangazo hili limetolewa na:-

**Emmanuel Johnson**
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**KISHAPU**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
YA KISHAPU